# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 12*

### KUMBUKUMBU YA KOZI YA TUJIFUNZE BIBLIA.

Somo hili ni hitimisho la masomo 11 uliyojifunza. Masomo hayo ni msingi thabiti wa kuendelea kujua umuhimu wa kujifunza neno la Mungu na, kulifuata. Utabarikiwa sana na, utaendelea kubarikiwa kadri utakavyotia nia ya kujifunza zaidi, kusudi upate cheti chako kwa heshima ya kuhitimu (kujifunza) msingi wa neno la Mungu, unatakiwa kujibu maswali yote katika somo hili: -

Mambo uliyojifunza **somo la kwanza**.

Umejifunza Biblia ilivyoandikwa, Umejifunza Biblia imetoka kwa Mungu,Umejifunza mafundisho kuhusu mambo ya sayansi,Umejifunza mambo yaliyo tabiriwa katika Biblia, Umejifunza sababu ya kuamini Biblia ni kitabu cha Mungu kwa Wakristo wa karne ya kwanza.

**Maswali.**

1. Neno Biblia (biblos) asili yake ni Kiyunani tafsiri yake katika Kiswahili ni ____________________
2. Nani alimwongoza mwanadamu kuandika Biblia? ____________________
3. Kuna tofauti gani kati ya Biblia na vitabu vya wanadamu? ____________________
4. Biblia inasema wazi kwamba dunia ilikuwa mviringo. Taja nabii aliyesema maneno hayo ____________________
5. Nabii Yoeli 2:28-32 alitabiri mambo saba ambayo yalitimizwa Agano Jipya. Taja kitabu na siku yalipotimizwa mambo hayo. ____________________
6. Taja sababu mbili zinazofanya tuamini kuwa Biblia ni kitabu cha Mungu ____________________
7. Kwa nini Biblia imekataza tusiongeze wala tusipunguze neno la Mungu? ____________________
8. Mtu asiye dumu katika mafundisho ya Kristo hana nini? ____________________

Mambo uliyojifunza **somo la Pili.**

Agano la kale na idadi ya vitabu vyake, Maana ya Agano Jipya, Lugha iliyotumika kuandika Biblia Agano la Kale na Agano Jipya, Mungu alivyoumba mbingu na nchi, Kuumbwa kwa Adamu na Hawa, Nyoka (Ibilisi) alivyo mdanganya hawa, Kaini alivyomuua ndugu yake Habili, Mungu alivyo mwambia Nuhu atenegeneze safina itakayomwokoa yeye na familia yake, Mungu alivyomwahidi Ibrahimu kuwa Taifa kubwa, Kuhusu Isaka, Yakobo na Esau, Makabila 12 yaliyotokana na uzao wa Yakobo, namna

wana wa Israeli walivyopokea Torati (sheria) katika mlima sinai, namna wana wa Israeli walivyovunja amri za Mungu walipokuwa jangwani, umejifunza, Jinsi Waisraeli walivyo taka Mfalme, Ufalme ulivyo gawanyika baada ya Sulemani kufa, Manabii wa Agano la Kale walivyotabiri kuhusu mwokozi Yesu Kristo.

**Maswali.**

1. Kwa nini Mungu alimkubali Habili na sadaka yake? (Ebr 11:4) ____________________
2. Taja lugha mbili za asili zilizo tumika kuandika Biblia. ____________________
3. Kwa nini Kaini alimuua Habili? ____________________
4. Je, Habari za wokovu wakati wa gharika mfano wake ni nini leo? (1Pet 3:20 -21) ____________________
5. Mungu aliposema jamaa zote za dunia watabarikiwa katika lbrahimu alikuwa anamaanisha nini? ____________________
6. Makuhani wote wa Agano la Kale walitoka katika kabila gan? ____________________
7. Taja wafalme wawili waliotawala baada ya Sulemani kufa.
    i. Ufalme wa Israeli____________________
    ii. Ufalme wa Yuda____________________

Mambo uliyojifunza **somo la Tatu**.

Katika mambo uliyojifunza, kuzaliwa kwa Yesu, kazi na kifo chake na kufufuka kwake kwa kifupi ndiyo Injili (habari njema). Injili ni vitabu vya Mathayo, Luka, Marko. Yohana, Matendo ya Mitume, Nyaraka zote, na ufunuo ili kuelewa uwiano sawa na uelewa.

**Maswali.**

1. Taja vitabu ambavyo vinaeleza maisha ya Yesu Kristo. ____________________
2. Taja kitabu kilicho tabiri kwamba Bikira atachukua mimba, atamzaa mtoto mwanamume. ____________________
3. Taja mambo matatu ambayo Shetani alimjaribu Yesu Kristo ____________________
4. Taja malengo ya Mungu kumwezesha Kristo kufanywa miujiza. ____________________
5. Kanisa gani ambalo Yesu aliahidi kulijenga? ____________________
6. Mwanzo Mungu alitabiri kwamba uzao wa mwanamke utamponda kichwa Shetani, Je, unabii huu ulitimizwa wakati gani? ____________________

7. Vitabu Ishirini na moja vilivyoandikwa “waraka mmoja” vinaitwaje? ____________________

8. Taja nyaraka; moja inayoonyesha kuwa hatuko chini ya sheria za Musa, na ya pili inaonyesha jinsi Agano la Kale lilivyoondolewa ____________________

Mambo uliyojifunza **somo la Nne**.

Umejifunza Agano la Kale na Amri. Agano la Kale na Amri kumi yote yameondolewa, kulitumia kwa halali neno, je, Torati imeondolewa, Kwa nini Yesu alishika sheria za Musa, hatuwezi kushika sheria za Yesu na za Musa, kwa nini tunasoma Agano la Kale.

**Maswali.**

1. Kutumia kwa halali neno la kweli maana yake nini. ____________________

2. Yesu Kristo alipo sema “hakuja kutangua torati au manabii” bali kutimiliza. Je, alikuwa anamaanisha nini? ____________________

3. Torati ilikuwa kiongozi kutuleta wapi? (Mbinguni, kwenye dini, kwa Kristo, kwa viongozi wetu wa dini) ____________________

4. Eleza sababu moja tu kwa nini Yesu aliishika Torati? ____________________

5. Torati ya Musa iliwatenga watu katika makundi mawili. Yataje makundi hayo. ____________________

6. Kuna tofauti gani kati ya Agano la Kale, Amri kumi, Torati na Sheria? ____________________

7. Eleza faida mbili za Wakristo kusoma Agano la Kale. ____________________

8. Yesu Kristo ana mamlaka yote Mbinguni na Duniani. Taja amri ambayo alituachia tuishike ____________________

Mambo uliyojifunza katika **somo la Tano**.

Umejifunza kuhusu umoja, Kanisa la Kristo, Madhehebu na majina yao, mwanzo wa Kanisa la Kristo, Kanisa halikujengwa juu ya Petro, mkuu wa Kanisa na, makao makuu ya Kanisa.

**Maswali.**

1. Taja kanisa ambalo Yesu Kristo alisema atalijenga. ____________________

2. Kwa nini watu wengi hawataki kujifunza na kuingia katika Kanisa? ____________________

3. Eleza, nini maana ya madhehebu kama ulivyojifunza. ____________________

4. Eleza sababu mbili kubwa zinazosababisha madhehebu kuwepo kwa mjibu wa Mtume Paulo katika lKor. 1:10-13 ____________________

5. Je, katika madhehebu yote duniani ni dhehebu lipi ambalo Yesu Kristo alisema atalijenga? ____________________

6. Kanisa la Korintho, Efeso, Ikonio, Filipi na, mahali pengine yalikuwa yana aina moja ya imani? Kama jibu lako ni ndiyo eleza kwa nini, kama hapana eleza kwa nini. ____________________

7. Je, kati ya Petro, Yohana, Musa, Yakobo, na Yesu Kristo nani msingi na kichwa cha kanisa? ____________________

8. Baada ya Yesu Kristo kupaa kwenda mbinguni, siku ya hamsini (sikukuu ya mavuno ya Wayahudi) je, ni kanisa gani lilianzishwa? La Kristo au la Pentekoste? ____________________

<u>Mambo uliyojifunza katika **somo la Sita**</u>

Umejifunza kuhusu nifanye nini ili niokoke, Imani peke yake haitoshi. Imani inatakiwa iwe na matendo gani, Umuhimu wa ubatizo wa maji mengi, Makosa mengine wanayoyatenda watu, Maana ya kupata wokovu kwa njia ya ubatizo

**<u>Maswali.</u>**

1. Mungu alimuumba mwanadamu kwa upendo lakini baadaye akafarakana naye (Mungu). Taja sababu ambayo imefanya Mungu afiche uso wake. ____________________

2. Je, kati ya watu wafuataо ni yupi ambaye Mungu alimtuma duniani aokoe wanadamu? Yohana Mbatizaji, Yesu Kristo au Musa? ____________________

3. Je, watu wote wanao mwamini Yesu Kristo wataokoka? Kama ndiyo toa sababu, kama hapana toa sababu ____________________

4. Je, mtu akimwamini Yesu Kristo kuwa ni Bwana na mwokozi wa maisha yake atakuwa ameokoka? ____________________

5. Je, maji mengi yana umuhimu gani katika Ubatizo? (1 Pet 3:20-2 1) ____________________

6. Je, kuna tofauti gani kati ya ubatizo wa Yohana na ubatizo wa Yesu? ____________________

7. (a) Taja matendo au mambo matano yanayopaswa kufanyika ili mtu aokolewe, ____________________

   (b) Eleza kwa nini watu wengine wanasema ubatizo ni kutimiza haki yote ____________________

8. Soma maneno yafuatayo “Aaminiye na kuokoka atabatizwa, atahukumiwa asiye amini” Kama yana ukweli sema “ndiyo” kama hayana ukweli yarekebishe (Marko l6:16) ____________________

Mambo uliyojifunza katika **somo la Saba**.

Umejifunza kuhusu watoto wadogo wabatizwe? Dhambi ya Adamu na kifo cha kimwili, Yesu mkombozi wa wenye dhambi, watoto wachanga wasibatizwe.

**Maswali.**

1. Toa sababu mbili kwa nini watoto wadogo wasibatizwe? (Marko 10:13-16) ____________________
2. Roho zote ni mali ya Mungu Je! Ni roho gani itakayohukumiwa na Mungu? (Eze 18:1-4) ____________________
3. Je! mwenye dhambi akizaa mtoto, mtoto huyo atakuwa na dhambi? ____________________
4. Adamu alipotenda dhambi alihukumiwa na kupewa adhabu na Mungu. Je. Leo sisi tunarithi vipi adhabu aliyopewa Adamu? ____________________
5. Roho zetu zinakufa kwa ajili ya dhambi ya nani? ____________________
6. Imani maana yake nini? ____________________
7. Je, mtoto mdogo anajuwa dhambi maana yake nini? toa sababu ____________________
8. Kwa nini Yesu alisema watoto wadogo ufalme wa mbinguni ni wao? ____________________

Mambo uliyojifunza katika **somo la Nane**.

Umejifunza kuhusu Maisha mapya ya Mkristo, Mwenye dhambi ni nani. Je, tuzifiche dhambi? Utu wetu wa kale umekufa, Mungu hana upendeleo, Upendo wa Mungu na wokovu, Tujilindeje na dhambi? Mkristo na mwili wake, Akiba ya haki.

**Maswali.**

1. Mtu akibatizwa akitenda dhambi yeye ni mtoto wa nani? ____________________
2. Maisha mapya ya Mkristo maana yake nini? ____________________
3. Ni ubatizo gani Yesu anaagiza watu wenye dhambi wabatizwe? ____________________
4. Utu wa kale maana yake nini? ____________________
5. Kwa nini Mungu hapendi mtu yeyote apotee katika dhambi? ____________________
6. Kwa nini siku ya Pentekoste Wayahudi waliamua kubatızwa hali walimchukia Yesu Kristo? ____________________

7. Mtu akibatizwa anakuwa nani? ____________________

8. Je, imani chanzo chake ni nini? (Rumi 10:17) ____________________

Mambo uliyojifunza katika **somo la Tisa**.

Umejifunza kuhusu Roho Mtakatifu na miujiza, Miujiza na ishara, Ubatizo wa Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu na Kornelio, Kukoma kwa miujiza. Miujiza ilikoma lini, Miujiza ya kisasa, Pamoja na maonyo.

**Maswali.**

1. Je, nani ambaye anaweza kupata Roho Mtakatifu? ____________________
2. Taja mtu ambaye hakufanya miujiza ingawa alikuwa na Roho Mtakatifu tangu tumboni mwa mama yake ____________________
3. Ni watu gani waliobatizwa katika Roho Mtakatifu siku ya pentekoste? ____________________
4. Taja Mtume ambaye alikufa kabla Yesu hajafufuka ____________________
5. Je, nani walikuwa na uwezo wa kuwawekea wengine mikono ili nao wafanye miujiza? ____________________
6. Taja mtu aliyepata Roho Mtakatifu bila ya kuwekewa mikono na Mitume ____________________
7. Miujiza na ishara ilikoma wakati gani? ____________________
8. Eleza tofauti iliyopo kati ya miujiza waliofanya Mitume 12 wa Yesu na Miujiza inayofanyika siku zetu za leo (Miujiza ya kisasa) ____________________

Mambo uliyojifunza katika **somo la Kumi**.

Umejifunza kuhusu Ibada ya Kikristo, Kuomba na kushukuru, Kuimba, Kuhubiri neno la Mungu, Kutoa changizo, Chakula cha Bwana au meza ya Bwana (Ushirika Mtakatifu).

**Maswali.**

1. Taja watu wa kwanza katika historia ya Biblia kumwabudu Mungu. ____________________
2. Nini maana ya ibada ya bure (Mt. 15:8-9) ____________________
3. Wakristo wanatakiwa kumwimbia Mungu katika ibada kwa kutumia nini? ____________________
4. Kuna tofauti gani kati ya kutoa, changizo na zaka? ____________________
5. Nini maana ya chakula cha Bwana au ushirika Mtakatifu? ____________________

6. Kwa maagizo ya Mungu (Biblia) Wakristo wanatakiwa kushiriki chakula cha Bwana siku gani? ____________________
7. Taja sababu tatu kwa nini wakristo wanatakiwa washiriki chakula cha Bwana ____________________
8. Je, nani ambaye anastahili kushiriki chakula cha Bwana? ____________________

<u>Mambo uliyojifunza katika **somo la Kumi na moja**.</u>

Umejifunza kuhusu watumishi na waangalizi wa Kanisa, Mitume, Manabi, Wainjilisti, Wahubiri na Walimu, Wazee, Maaskofu, Waangalizi na Wachungaji, Mashemasi, Kuhani mkuu, Makuhani, na Wanawake katika Kanisa.

<u>**Maswali.**</u>

1. Kwa nini Wakristo walitaka kugawanyika katika karne ya kwanza? ____________________
2. Taja sifa nne za mtu aliyetakiwa kuwa mtume baada ya Yuda Iskariote kufa. ____________________
3. Kuna tofauti gani kati ya Askofu, Mchungaji, Mzee, Pastor na Mwangalizi? ____________________
4. Kwa maagizo ya Mungu Kanisa linatakiwa liwe na Wachungaji kuanzia wangapi? Tit.1:5; 1Pet.5:1 ____________________
5. Taja angalau sifa tano ambazo Askofu anatakiwa awe nazo. ____________________
6. Kila mtu Kanisani anaweza akawa Mchungaji? Kama ndiyo toa sababu, kama hapana toa sababu. ____________________
7. Kazi kubwa ya Kuhani mkuu ilikuwa nini? ____________________
8. Kwa mujibu wa Biblia mwanamke hawezi kuwa Askofu. Toa sababu ____________________

*************************************************************************************

Jina lako …………………………………………………
Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***
***Tanzania***